



MASENO UNIVERSITY
UNIVERSITY EXAMINATIONS 2013/2014

THIRD YEAR SECOND SEMESTER EXAMINATIONS FOR THE
DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION & BACHELOR OF ARTS
WITH INFORMATION TECHNOLOGY

(MAIN CAMPUS)

AKI 312: TRANSLATION II (TAFSIRI II)

Date: 22nd July 2014

Time: 2.30 – 4.30 pm

MAAGIZO:

- Jibu maswali MATATU pekee, swali MOJA kutoka sehemu A na MAWILI kutoka sehemu B.



MAIN CAMPUS
[TRIMESTER, MAY-AUGUST, 2014]

AKI 312: TRANSLATION II (TAFSIRI II)

MAAGIZO: JIBU SWALI MOJA KUTOKA SEHEMU YA (A) NA MASWALI MAWILI KUTOKA SEHEMU YA (B).

SEHEMU YA (A) KILA SWALI [ALAMA 26]

1. Tafsiri makala ifuatayo katika Kiswahili sanifu. **[Alama 26]**

'Swahili language planning agencies (LPAs) in Tanzania Mainland and Zanzibar have each published authoritative monolingual Standard Swahili dictionaries that lead to two distinct standard varieties of Swahili. The *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS) by TUKI1 (now TATAKI2) of 2004 and the *Kamusi ya Kiswahili Fasaha* (KKF) by BAKIZA3 of 2010 provide evidence that two varieties of Standard Swahili in the form of *Kisanifu* and *Kifasaha* are currently being formalised.

Based on Haugen's (1966, 1987) classical framework for deriving a standard language and by using acrolectal textual evidences from Tanzania Zanzibar and Tanzania Mainland formal writings, this paper claims that the two varieties are indeed formal standard codes. Editors, teachers of Swahili as a foreign language, lawyers, journalists, translators and users are advised to consider these variations in their contact with modern Standard Swahili language.'

[Kipacha, 2012]

2. Dhihirisha kufaulu au kutofaulu kwa tafsiri ya majina ya wahusika katika *Shamba la Wanyama* [Fortunatus Kawegere, 1967] kutoka *Animal Farm* (George Orwell, 1945). **[Alama 26]**
3. Tafsiri makala ifuatayo kutoka Kiswahili hadi Kiingereza. **[Alama 26]**

ONYESHO LA 2

Katika ofisi ya Profesa Magige. Taa zinapowaka tunamwona Profesa Magige, akiongea na walimu wengine wawili pamoja na mwanafunzi mmoja:

Magige: (Kwa *tahadhar*) Mabibi na mabwana; nina hakika mnaifahamu jinsi ninavyoathamini urafiki wenu.

Gichena: *(Kwa unyenyekevu)* Huna haja ya kusema zaidi bwana. Kuteuliwa kwako hapa imekuwa ni kama ndoto iliyojibiwa kwa muujiza wa Mungu...

Wankuru: *(Anajipendekeza)* Hatimaye hata sisi tumekumbukwa. Unafahamu kabila letu limekuwa nyuma sana.

Magige: *(Akiwatahadharisha zaidi)* Ninaelewa hivyo lakini ni muhimu tujichunge na kauli zinazoweza kutinga matakwa na mapendekezo yetu.

Nyambura: Ni lazima tujue kwamba wanafunzi wana ari kubwa ya kumwagamiza Profesa.

Gichena: *(Kwa dhati)* Hao watashindwa. Tutawafukuza wote wasiotii. Ni lazima wajue kwamba Chuo Kikuu si pori. Kuna sheria...

Nyambura: Wanafahamu hivyo lakini wanatamani sana kuvuruga. Wana chuki na uongozi.

Wankuru: Na hili ndilo jambo ambalo linanititiza. Silielewi...Kwa nini wanafunzi wa Chuo Kikuu hawawezi kushirikiana nasi katika kuendeleza maslahi ya watu wetu.

Magige: Ni vizuri tusihamaki. Nilipokuwa mwanafunzi enzi zangu niliongoza mgomo...

Gichena: Ama. Ndio unasema nini sasa? Umetuita kuja kufanya nini?

Magige: *(Anakumbukia)* Ilikuwa ni zamani na sasa ninafahamu kabisa kuwa hatukuwa na sababu ya kugoma. Lakini...

Gichena: *(Anamkata kauli)* Huna haja ya kusema hivi. Wenzagu wakisikia ushuhuda huu watafurahi.

SEHEMU YA (B) KILA SWALI [ALAMA 22]

4. a. Eleza dhana ya visawe. **[Alama 02]**
 - b. Ukitoa mifano mwafaka, fafanua aina mbalimbali za visawe. **[Alama 20]**

5. Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza taratibu zifuatazo za tafsiri: **[Alama 22]**
 - a. Uhawilisho
 - b. Tafsiri fululizo
 - c. Upanuzi
 - d. Ufupisho
 - e. Unukuzihati

6. Tathmini michango ya fonolojia na mofolojia katika matumizi ya tafsiri tohozi mintarafu tafsiri ya majina anuwai ya nchi. **[Alama 22]**